MUHTASARI WA MAFUNDISHO KUHUSU UKRISTO. Christian Doctrine.

Mafundisho ya ukristo ni mafundisho ya Biblia. Mafundisho haya mara kwa mara yanaweza kuwa magumu sana na wakati mwinngine kuleta kutakubaliana. Katika kufundisha kwako, hakikisha kwamb unawapatia wanafunzi nakala ili waweze kujisomea na kuelewa Zaidi. Pia hakikisha kwamba unaepukana na ugonvi.

Unapokuwa unasoma nakala hizi, kumbuka kwamba huenda mambo haya umejifunza wakati mwingine kama ulipokuwa unajifunza kuhusu Agano la Kale na Agano Jipya. Mafundisho ya Ukristo yanajumlisha mafundisho memngi ambayo yamo katika Biblia nzima. Mafundisho haya yanajumlishwa pamoja ili tuweze kuelewa vyema kabisa mambo ya muhimu ya Biblia.

Utangulizi

I. Dini

1. Maana ya dini.

A. Ibada ya kuabudu Mungu au miungu.

B. Kujtolea katika Imani au kutilia mambo fulani manani

C. Imani tofauti ambazo wengi wanajitolea kwake kwa bidi sana. Hii Imani inaweza kuwa ya uongo kama Uislamu au dini nyingine yoyote. Waislamu wanaamini sana katika miungu yao, kiwango kwamba wako tayari kujitoa uhai kwa ya miungu yao. Wakristo wanamwamini sana Mungu wao kiwango kwamba wanajitoa kabisa kumtumikia kila wakati na katika hali zote.

2. Dini ni jambo la ulimwengu wote. Popote kuna wanadamu, utapata dini hapo. Hii inaonyesha wazi kwamba mwanadamu ana kiu cha kumjua Mungu na kuwa na husiano Naye.

3. Jinsi dini ilivyo. Je, dini ni nini? Je, dini inakaaje?

A. Dini ni jambo la dhamira na la kujitoloea katika kumwabudu Mungu. Ni wakati wa kuonyesha asante kwa Mungu katika kumwabudu Mungu na kumtolea idada ya upendo. Ni Mungu ambaye anaongoza ibada ya kweli ambayo inakubalika machoni pake (Kumbukumbu la Torati 1:12-13; Zaburi 111:10, Mhubiri 12:13 na Yohana 6:29).

i. Jambo la kuzingatia: Dini ya kweli ni ile ambayo Mungu mwenyewe anaiongoza. Shida kubwa ni kwamba, kila mara mwanadamu ndiye anataka kuamua Jinsi Mungu atakavyofanya. Kwa ufupi ni kwamba, mwanadamu anataka kila mara kuwa na miungu yake. Mfano ni dini ya Kiislamu au madhehebu ya kiroho. Dini ya kweli inatoka kwa Mungu. Mwanzo 1:27, tunasoma kwamba Mungu alimwumba mwanadamu katika mfano wake na alimpa uwezo wa kuwa na uhusiano Naye.

4. Dini ni jambo la moyo. Mungu huwa hajali mambo ya nje ya dini. Mungu hutaka tumwabudu kwa kweli kutoka ndani ya mioyo yetu (Mithali 4:23 and Amosi 5:21-24).

A. Katika Aganoi Jipya, dini ya kweli inatokana na injili ya kweli na wala si kwa kutii sharia. Dini ya kweli hutoongza katika Imani na kumcha Mungu. Hii ina maana kwamba dini ya kweli msingi wa wake ni Mungu ambaye ametudhihirishia mwanawe Kristo yesu.

5. Chanzo cha dini.

A. <u>Wanadamu wenyewe wamevumbua dini kulingana na mawazo yao. Kwa mfano uganga au dini za kiroho.</u>

B. Je, Biblia inafunza nini kuhusu dini? Biblia inafundisha kwamba dini ya kweli inatokana na Mungu. Mwanadamu wa kwanza alikuwa na uhusianoi na Mungu wa karibu sana.

II. Ufunuo

1. Ufunuo kutoka kwa Mungu ndio unatuwezesha kumfahamu Mungu. Ufunuo inamaanisha kuweka wazi kile ambacho kilikuwa kimefishika. Mungu amejifunua kwetu kwa njia mbili: kupitia kwa kiumbe na kwa Biblia.

A. Mungu amejifunua kwetu kupitia kwa kiumbe. Vyote ambavyo vimeumbwa na kupitia kwa matokeo ya wanadamu na historia, Mungu anajifunua kwetu (Zaburi 19:1, 2; Warumi 1:19, 20; 2:14, 15). Njia ya kujifunua kwetu na Mungu huwa haituelezi kile kitu kabisa na haiwezi kutufanya tupate maisha ya kiroho. Kwa sababu hii hatuwezi kujua Mungu vyote au kupata

uzima wa milele. Yale ambayo tufahamu kupitia kwa njia ya Mungu kujifunua kwetu haitoshi kutuletea uzima wa milele.

i. Kupitia kila kitu ambacho Mungu ameumba, tuona Mungu akijileza kwetu. Kiumbe kinadhihirisha nkwamba Mungu upo, lakini ufahamu huu, hautoshi kututleat kwa Kristo kwa Imani (Zaburi 19:1-2, Warumi 1:18-20).

B. Mungu amejidhihirisha kupitia kwa Biblia. Njia hii inatuongoza katika wokovu kupitia kwa Kristo. Biblia inatufunza kwamba ni Mungu ambaye ametuptia Biblia na kwamba Biblia ni neno lake (Hesabu 12:6-8, Waebrania 1:1 na 2 Petero1:21).

i. Umuhimu wa Biblia. Baada ya Adamu na Hawa kuanguka katika dhambi, kila kitu kiliharibiwa na dhambi hata mwanadamu. Kwa sababu hii Mungu alitupatia neno lake ili atueleze kuhusu wokovu ambao ungekuwa njia ya kuondoa mwanadamu katika dhambi. Tunaweza tu kujifunza kuhusu Yesu kupitia kwa Biblia pekee (Warumi 10:9-10).

ii Njia ya Biblia.

a. Mungu alijidhihirisha kwa njia tofauti tofauti kama katika moto, mawingu na moshi (Kutoka 3:2; 33:9; Zaburi 78:14; 99:7); katika mawimbi makali (Ayubu 38:1; Zaburi 18:10-16) katika sauti tulivu (1Kings 19:12).

b. Mungu alizungumza na watu waziwazi. Yeye alizungumza na Musa na Waisr aeli (Kumbukumbu la Torati 5:4). Mara nyingine anazungumza na manabii kwa njia ya Roho Mtakatifu (1 Petero 1:11). Pia alijidhihirisha katika ndoto na maono (Hesabu 12) Sauti ya Mungu ilisikika wazi (Hesabu 12:6; 27:21; Isaya 6). Agano Jipya linatufundisha kwamba Kristo ndiye mwalimu mkuu kutoka kwa Mungu ili atuonyeshe mapenzi ya Mungu (Yohana 14:26).

c. Miujiza. Miujiza ya Biblia haifai kuchukuliwa kama jambo la kuwafurahisha tu watu au kuwezwa kufanywa na wengine. Miujiza ilitumika na Mungu kujidhihirisha kwetu. Miujiza ilidhihirisha huduma wa Kristo na Kristo ni nani. Miujiza kusudi lake ilikuwa kuwafanya watu wamwamini Kristo (Yohana 11:44-45, Matendo ya Mitume 9:36-42). Leo Mungu bado anafanya nmiujiza lakini wakati anapotaka mwenyewe. Wokovu ni muujiza mkuu kutoka kwa Mungu.

III. Mungu anajidhihirisha kwetu kupitia kwa Biblia. Chochote ambacho tunafaa kujua kumhusu Mungu kinapatikana katika Biblia. Biblia ni neno la Mungu; haina makossa yoyote na ina mamlaka (1 Wakorintho 2:13; 2 Timotheo 3:16). Biblia imakamilika. Kumbuka kwamba ni Biblia pekee ambayo inatueleza kuhusu Mungu na kutufunza kuhusu kile ambacho Mungu anataka tujue.

1. Tunaposema maandiko huwa tunamaanisha Biblia. Biblia ni neno la Mungu. Kila kitu katika Biblia ni neno la Mungu na linafaa kwa kila mutu. Biblia ndio kanuni ya Imani na maisha ya ukristo kwa kila mwanadamu. Tunapaswa kuitii Biblia yote. Waandishi wa Agano la kale mara kwa mara walisisitiza kuandika kile ambacho Mungu alikuwa amesema (Kutoka 17:14; 34:27; Hesabu 33:2; Isa 8:1,30:8; Yeremia 25:13; 30:2; Ezekieli 24:1;Danieli 12:4,Hab 2:2. 2Timotheo 3:16).

2. ASili ya maandiko au Biblia.

A. Kuna mambo mawili ya uongo kuhusu Biblia.

i. Kuna wazo kwamba wakati Biblia ilipokuwa inaandikwa, Mungu alikuwa anasema wakati huo huo, mtu akiandika. Wazo hili linasisitiza kwamba waandishi walikuwa kama kalamu mikononi mwa Mungu. Wazo hili linafundisha kwamba waandishi hawakutumia fikira zao walipokuwa wanaandika. Ukweli ni kwamba waandishi wa Biblia mara kwa mara walikusanya habari ambazo waliziandika na wala hawakukaa tu Mungu anazungumza na wao waliandika chini (1 Wafalme 11:41; 14:29; 1 Mambo ya Nyakati Chr 29; 29; Luka 1:1-4).

Pia katika sehemu zingine za Biblia, walinukuu mawazo yao na walitumia mitindo yao tafauti ya uandishi.

ii. Wazo linguine la uongo ni kwamba waandishi wa Biblia walipewa nguvu na uwezo wa kuona mambo kwa njia ya ajabu na hali yao ya kiroho iliinuliwa juu kabisa. Wazo hili si la ukweli.

B. Wazo la kweli ni kwamba waandishi wa Biblia waliandika wakiktumia talanta zao, hekima yao, masoma yao na mitindo yao tofauti ya uandishi. Lakini walipokuwa wanaandika, Roho

Mtakatifu aliwaongoza kuandika kile ambacho ni neno la Mungu. Kwa sababu hii Biblia ni neno la Mungu.

C. Kiasi cha Maandiko.

i. Kusema kwamba Biblia yote si neno la Mungu, ni kusema uongo kwa sababu kila neno katika Biblia ni neno kutoka kwa Mungu. Biblia yote kwa pamoja ni neno la Mungu.

ii. Biblia yote ni neno la Mungu, Agano la Kale na Agano Jipya. Yesu mwenyewe na Mitume wake mara kwa mara walinukuu Agano la kale na kuhakikisha kwamba ni Neno la Mungu (2Peter 3:16, 2Timotheo 3:16).

3. Biblia yote inakubalika na kanisa kama njia ya pekee ambayo Mungu anaitumia kuzungumza nasi leo.

III. Mafundisho ya Biblia kuhusu Mungu

1. Je, ni jinsi gani Mungu alivyo? Ukweli ni kwamba hatuwezi kabisa kueleza jinsi Mungu alivyo, lakini tunaweza tu kusema kulingana na jinsi Mungu mwenyewe amejieleza katika Biblia. Mungu ni mtakatifu kabisa na Yeye ni wa milele. Ukweli huu kuhusu Mungu unafafanua mambo haya yafuatayo:

A. Mungu hana mwili na kwa hivyo hawezi kuonekana kwa macho ya kiasili (Yohana 4:21-24 na 1Timotheo 6:16). Kwa sababu hatuwezi kumwona Mungu, Mungu ameamua kujifunua kwetu kupitia kwa Kristo.

B. Mungu ana hekima yote na hahitaji hekima au kufahamu kwa mtu au kiumbe chochote. Lakini Yeye ana uhusiano na watu kwa sababu sisi ni viumbe vyake (Malaki 2:10; Isaya 43:1,7,2; 44:2,21,24).

C. Mungu ni mkamilifu kabisa. Yeye si kama viumbe ambavyo vimeadhiriwa na dhambi. Yeye ni Zaidi ya viumbe vyake. Yeye hana dhambi yoyote au makosa yoyote (Kutoka 15:11, Zaburi 147:5).

D. Mungu ni Mungu, haishi kwa sababu anasaidwa na lolote. Yeye anaishi kwa sababu Yeye ni Mungu.

2. Kuna majina mengi ya Mungu katika Biblia.

A. Majina ya Mungu katika Agano la kale:

i. Yeye ni Mungu mwenye nguvu zote (Mwanzo 1:1, Kumbukumbu la Torati 10:17).

ii. Mungu anatawala kila kitu (Zaburi 86:8).

iii. Mungu ni mkuu na atawala kila kitu (Kutoka 6:3).

iv. Yeye ni Yehova, maana yake ni kwamba Mungu ni wa milele na ana nguvu zote Jehovah (Kutoka 3:14-15).

v.Mimi ndimi (Kutoka 3:14)

vi. Yeye ni Bwana (Kutoka 6:3).

B. Majina ya Mungu katika Agano Jipya

i. Mungu (Mathayo 1:23)
ii. Bwana (Mathayo 7:21)

iii. Baba (1 Wakorintho 8:6).

iv. Mwanzo tena mwisho (Ufunuo 22:13)

IV. Jinsi Mungu alivyo

1. Kuna sifa ambazo ni za Mungu pekee. Yaani hakuna kiumbe kingine kina sifa na uwezo kama wake.

A. Mungu hategemei yeyote au lolote. Yeye hamhitaji yeyote ili aendelea kuwepo. (Yohana 5:26, Warumi 11:33-36).

B. Mungu habadiliki kamwe. Yeye ni kamili (Malachi 3:6).

C. Mungu hapimiki. Ukamilifu wake hauna mwisho na wala hauwezi kupimika. Mungu hazuiliwi kwa lolote.; hekima yake, upendo, utakatifu, yote hayana mwisho (Ayubu 11:7-10; Zaburi 145:3). Yeye wakati uko mikononi mwake na hapungukiwa na wakati (Zaburi 90:2; 102:12). Yeye upo kila mahali (1 Wafalme 8:27; Zaburi 139:7-10, Isaya 66:1; Yeremia 23:23-24; Matendo 17:27-28).

i. Utakatifu wa Mungu hauwezi ukapimika. Yeye ni Mtakatifu na hivyo ndivyo alivyo (Ayubu 11:7-11).

ii. Mungu ni wa milele (ZAburi 90:2, Isaya 41:2). Hii inamaanmisha kwamba Mungu hana mwanzo wala mwisho. Mungu amekuwepo siku zote. Je, sisi wanadamu tunafahamu hili kwa njia gani? Ukweli ni kwamba hili ni gumu kuelewa, lakini tunapaswa kuamini hivyo.

a). Kuna mambo mengine katika Biblia ambayo hatuwezi kuelewa hasa, kama kuwepo kwa Mungu milele na Mungu wa Utatu. Kumbukumbu la Torati 29:29 na Isaya 55:8-9, tunasoma kwamba Mungu hajaeleza kila kitu na pia kwamba Yeye huwaza tofauti nasi. Hili ni lazima tukubali kwa Imani.

iii. Mungu yupo kila mahali (Zaburi 139:7-10).

D. Mungu hana sehemu tofauti kama mwili, na nafsi. Yeye hawezi kugawanywa. Mungu wa Utatu hawezi agatenganishwa, kwa sababu Mungu ni mmoja.

2. Kuna baadhi ya mambo anayafanya na pia ana mwezesha mwanadamu pia. Lakini hata kama mwanadamu ana baadhi ya mambo haya, ukweli ni kwamba amepungukiwa. Mfano wa mambo haya ni kama:

A. Kama wanadamu tumepungukiwa katika kufahamu mambo. Kwa mfano hatumfahamu Mungu kabisa. Mungu ndiye anajua kila kitu.

B. Hekima ya Mungu (Warumi 11:33, 1 Wakorintho 2:7). Mungu anajua kila kitu. Lakini sis hatujui kila kitu (Mithali 2:6).

C. Uzuri wa Mungu. Kila wakati Mungu ni mzuri na uzuri wa Mungu unatokana naye (Zaburi 100:5, 36:6, 104:21, Mathayo 5:45). Bila Mungu kumsaidia mwanadamu, mwanadamu ataendelea kuwa mwovu. Wakristo wana uzuri ambao wanatoa kwa Mungu, hata kama wao bado hufanya dhambi wakati mwingine.

D. Mungu amedhihirisha upendo wake kwa njia ya mtoto wake (Yohana 3:16 na 17)

i. Neema ya Mungu ni upendo wa Mungu kwetu ambao hatustahili (Waefeso 1:6-7).

ii. Mungu amedhihirisha huruma wake katika upendo wake kwetu (Luka 1:54).

iii. Mungu anatuvumilia sana (Warumi 2:4).

E. Utakatifu wa Mungu unamaanishi kwamba Yeye na kiumbe ni totafuti kabisa (Warumi 15:4). Yeye ni mkuu sana kuliko kiumbe chake na anaisha katika utukufu mkuu (Exodus 15:11, Isaya 57:15). Yeye hana dhambi yoyote na ndani mwake hamna dhambi. (Ayubu 34:10; Isaya 6:5; Habakuki 1:13).

F. Mungu ni mwenye haki. Hii inamaana kwamba Mungu hatagemei chochote kuendelea kuwa mtakatifu na kwamba anajitegemea mwenyewe. Yeye huweka serikali na kuifanya izingatia sharia katika kuendelea kushughulikia wanaichi wake. Yeye hufanya wale ambao wanaishi kwa utiifu waweze kuzawadiwa (Zaburi 99:4; Isaya 33:22; Warumi 1:32).

i. Mungu ametupatia sharia ambayo itatuongoza katika maisha yetu ya kila siku (Warumi 1:32). Mungu anaahidi zawadi kwa wale ambao wanatii na hukumu kwa wale ambao wanakata kutii.

ii. Haki yake inadhihirika katika kuwazawadia malaika na wanadamu (Warumi 2:7). Mungu hupeana vitu vizuri kwetu kwa sababu anatupenda.

iii. Mungu atawahukumu wale wote ambao wanakataa kutii (Warumi 2:9).

G. Mungu husema ukweli. Yeye ndiye Mungu wa kweli na Yeye husema ukweli. Yeye kila wakati ni mwaminifu na hawezi kamwe kusema uongo (Hesabu 23:19).

H. Ukuu na utawala wa Mungu.

i. Mapenzi ya Mungu katika utawala wake (Danieli 4:35). Mungu hufanya jinsi anavyotaka.

a. Kumbukumbu la Torati 29:29, tunasoma kwamba Mungu ana mambo fulani ambayo ameyaficha na mengine ambayo ameyafunua wazi kabisa. Warumi 11:33-34, tunasoma kuhusu mambo ya Mungu ya siri. Warumi 12:2, tunasoma kuhusu mambo ambayo Mungu ameyafunua wazi.

b. Mungu anahuru ya kuumba na kupenda yeyote ambaye anataka kupenda (Warumi 9:15-18).

c. Mungu hahusiki na dhmabi kamwe lakini Yeye hutuacha tuchague katika dhambi na wema. Yeye hafurahi kamwe wakati tunaendelea katika dhambi.

ii. Utawala mkuu wa Mungu unamaanisha kwamba Mungu anaweza kufanya chochote ambacho anataka wakati wowote (Yeremia 32:27). Lakini pia tukumbuke kwamba kuna mambo ambayo hawezi akafanya kama kudanganya wala kubadilika (Hesabu 23:19).

3. Je, kwa nini ni muhimu kujifunza jinsi Mungu alivyo?

A. Hii inatusaidia kufahamu jinsi Mungu wetu alivyo mkuu na jinsi wokovu wake ulivyo zawadi kuu sana kwetu (Kumbukumbu la Torati 7:21; 10:17).

4. Je, tunapaswa kufanya nini ni ufahamu wetu kumhusu Mungu?

A. Hakikisha kwamba mambo haya yanakusaidia katika maombi yetu. Ni vyema sana katika maombi yetu kuelza Mungu kwamba kweli tunamfahamu, na tunampenda na tunamshukurua kwa jinsi alivyo. Anza maombi yako ukimsifu Mungu kwa jinsi alivyo.

B. Furahia katika Mungu mkuu.

V. Mungu wa Utatu.

1. Hakuna mwanadamu anaweza kueleza kabisa kuhusu Mungu wa Utatu Zaidi na jinzi Biblia inavyoeleza. Kumbuka kwamba hapo mwazoni tulisema kwamba hakuma mtu ambaye anaeleza kila kitu katika Biblia. Mungu ni mmoja, na Yeye ni Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu. Yeye ni mmoja na wala si watatu. Mungu wa Utatu ni mmoja katika nguvu, utukufu na hali.

B. Ukweli huu kumhusu Mungu, walimu wa uongo wanauchukia.
C. Katika Biblia nzima, hakuna mahali ambapo tunasoma neno Mungu wa Utatu. Lakini mafundisho kuhusu Mungu wa Utatu yamo katika Biblia nzima.

D. Mafundisho ya Agano la Kale kuhusu Mungu wa Utatu.

i. Mungu hujizungumzia akiwa Mungu wa Utatu (Mwanzo 1:26; 11:7 na Isaya 6:8).

ii. Roho Mtakatifu anazungumziwa akiwa Mungu mwenyewe (Isaya 48:16; 61:1; 63:10).

iii. Kuna mistari nyingi sana ambayo inazungumza kuhusu Roho Mtakatifu (Mwanzo 1:2, 4:38; 1 Samweli 10:6).

E. Agano Jipya linazungumza kuhusu Mungu wa Utatu.

i. Alitajwa wakati Kristo alikuwa anabatizwa (Luka 3:21-22).

ii. Alitajwa katika mafundisho ya Yesu (Yohana 14-16).

iii. Alitajwa katika kazi ya kueneza injili (Mathayo 28:19).

iv.Alitajwa katika Baraka za mitume (II Wakorintho 13:14).

v. Anatajwa katika Luka 1:35, I Wakorintho 12:4-6, na 1 Petero 1:2).

2. Mungu Utatu akizungmzia kila mmoja pekee yake

A. Mungu Baba anatajwa katika majukumu tofauti

i. Yeye ndiye chanzo cha kila ambayo imeumbwa (1 Wakorintho 8:6, Waefeso 3:14-15, Waebrania 12:9, Yakobo 1:17).

ii. Yeye ni Baba wa taifa la Israeli (Kumbukumbu la Torati 32:6, Isaya 63:16).

iii. Yeye Baba wa wale ambao wameokoka (Mathayo 5:45, Warumi 8:15).

iv. Yeye ni Baba wa Yesu (Yohana 1:14, Yohana 5:17-47).
B. Yesu, Mwana ndiye wa pili katika Utatu wa Mungu.

i. Yeye ni wa milele, hana mwanzo (Zaburi 2:7, Matendo 13:33). Yeye ndiye Mwana wa pekee.

ii. Mwana ni Mungu (Yohana 1:1, Warumi 9:5). Yeye ana nguvu zote kwa sababu Yeye ni Mungu.

iii. Kazi ambazo Mwana anazifanya (Yohana 1:3), vitu vyote vimeumbwa na vinaendelea kluwepo kwa nguvu za Mwana. Yeye ndiye nuru ambayo inapeana mwangaza kwa kila mwanadamu na kuondoa giza (Yohana 1:9).

iv. Kazi ya ukombozi aliifanya alipokuja hapa ulimwen guni kwa mwili wa mwanadamu na kuteseka, na kufa msalabani (Waefeso 1:3-14). Uhusiano wetu wa Amani na Mungu ni kupitia kwa Kristo Yesu (Yohana 14:6).

C. Mungu Roho Mtakatifu ndiye wa tatu katika Utatu wa Mungu.

i. Jinsi Roho Mtakatifu alivyo.

a. Yeye ni nafsi (Yohana 14:16, 17, 26; Warumi 8:26).

b. Yeye anachunguza (Yohana 14:26). Yeye anahisia (Isaya 63:19; Waefeso 4:30). Yeye ana mapenzi (Matendo 16:7).

ii. Roho Mtakatifu anahusiano na Mungu Baba na Mungu Mwana (Yohana 15:26, Wagalatia 4:6). Mistari hii inaonyesha kwamba Mungu wa utatu anafanya kwa pamoja.

iii. Uhusiano wa Roho Mtakatifu na Mungu Baba na Mungu Mwana ni wa karibu sana (1 Wakorintho 2:10-11).

iv. Wakati mwingine ni Kristo na wakati mwingine ni Roho Mtakatifu ambaye anaishi ndani mwa wale ambao wameokoka (Warumi 8:9-10, Wagalatia 2:20).

v.Roho Mtakatifu ni Mungu (Matendo ya Mitume 5:3-4, Mwanzo 1:2 na Mathayo 28:19).

vi. TKuna kazi katika biblia ambayo ni wazi kwamba ni kazi ya Roho Mtakatifu.

a. Kutoka 28:3 na 1 Samweli 16:13, Roho Mtakatifu huandaa watu kwa ajili ya kufanya kazi fulani.

b. Roho Mtakatifu hutusaidia kuelewa Biblia (I Wakorintho 2:13). Ni Yeye ambaye aliwezesha uandishi wa Biblia (2 Petero 1:21). Kwa sababu ya ukosefu wa Roho Mtakatifu katika mioyo ya wale ambao hawajaokoka, wao hawaelewi Biblia.
c. Roho Mtakatifu anaishi katika maisha ya wale ambao wameokoka. Ni Yeye ambaye anatupatia nguvu za kueneza neno la Mungu (Matendo 1:8). Yeye hutufariji (Matendo 9:31). Yeye huishi ndani mwetu (I Wakorintho 9:13). Roho Mtakatifu ni zawadi kutoka kwa Mungu aweze kutusaidia katika maisha haya.

d. Roho Mtakatifu ndiye analeta watu kwa Kristo (Tito 3:5).

VI. Kazi ya Mungu

1. Mungu amepanga kwamba kila kitu kifanyike kwa mpango na kusudi lake, ili aweze kutukuzwa. Mungu anampanga kwa kila kitu amacho kinafanyika (Isaya 46:10. Ayubu 23:13-14 na Mwanzo 50:20).

2. Mipango ya Mungu.

A. Mipango ya Mungu inaonekana katika hekima yake (Waefeso 1:11).

B. Ni lazima mapenzi ya Mungu yafanyike (Mithali 19:21 na Isaya 46:10).

C. Mungu huwa habadilishi mapenzi yake (Ayubu 23:13-14). Mungu ni Yule yule, jana leo n ahata milele.

D. Mapenzi yake hahitaji chochote kutoka kwetu ndipo yafanyike (Waefeso 2:8).

3. Baadhi ya mipango au mapenzi ya Mungu.

A. Mungu alitangulia kuchagua (Matendo 4:28; Yuda 4; Waefeso 1:4).

B. Mungu aliumba kila kitu (Mwanzo 1-2).

i. Wakati wa uumbaji ndiyo ulikuwa mwanzo wa kila kitu (Mwanzo 1:1).

ii. Mungu aliumba kila kitu bila chochote (Zaburi 33:9 na Waebrania 11:3).
C. Mungu aliumba hata vile vitu ambavyo havionekani kama malaika (Isaya 37:16).

i. Malaika: Ni viumbe vya Mungu (2 Samweli 14:20). Kuna malaika wazuri na wale wabaya (Yuda 1:6; Ufunuo 14:10). Malaika ni viumbe vya kiroho (Matendo 19:12).

ii. Mpangilio miongoni mwa malaika.

a. Makerubi wana majukumu ambayo tunayaona wazi katika Biblia (Mwanzo 3:24, Kutoka 25:18, II Samweli 22:11).

b. Maserafi pia wana majukumu (Isaya 6:2, 3 na 6).

iii. Majukumu ya malaika wazuri.

a. Wao humsifu Mungu mchana na usiku (Isaya 6, Ufunuo 5:11, Zaburi 103:20).

b. Wao humtumikia Mungu (Waebrania 1:14).

c. Wao hushereka wakati mwenye dhambi anaokoka (Luka 15:10).

d. Wao huleta Baraka kutoka kwa Mungu (Matendo 5:19).

e. Wao hutekeleza hukumu kutoka kwa Mungu (Mwanzo 19:1,13).

iv. Matendo ya malaika wabaya.

a. Hawa ni malika ambao waliumbwa na Mungu wakiwa watakatifu, lakini walichagua kuasi dhidi ya Mungu (2 Petero 2:4 na Yuda 1:6). Wao hufanya kinyume na Mungu na watu wa Mungu.

b. Shetani ndiye kiongozi wa malaika hawa (Mathayo 25:41). Yeye ndiye mwanzilishi wa dhambi (Yohana 8:44). Hawa malaika wabaya wana nguvu (Yuda 1:9).

4. Ulimwengu ambao tunaishi.

A. Tunaosma kuhusu kuumbwa kwa ulimwengu katika Mwanzo 1.

5. Mipango ya Mungu. Hii inamaanisha kwamba Mungu anatawala ulimwengu wote na kila kitu kilichi ndani. Yeye ndiye anaongoza kila kitu ambacho kinafanyika katika ulimwengu huu. Huwa hatutegemei bahati, bali Mungu pekee (Mathayo 6:25-34). Kila wakati Mungu upo pamoja nasi na kiumbe chote. Yeye anatawala kila kitu. Hakuna chochote ambacho kinafanyika bila mapenzi yake. Chochote ambacho kinafanyika, ni Mungu ambaye anakubali kifanyike (Mathayo 10:29 na Matendo 2:23 na Isaya 45:7).

A. Matendo ya Mungu katika mipango yake, ni matakatifu, yenye hekima na yenye nguvu. Yeye hutawala na kudhibitikiumbe chake chote. Mungu anaendelea kulinda na kuweka kiumbe chake chote (Zabiru 136:25; 145:15; Nehemia 9:6, Matendo 17:28 na Wakolosai 1:17. Ulimwengu uko mikononi mwa Mungu na Yeye ambaye anatawala kila kitu.

B. Mambo matatu kuhusu kutawala na mipango ya Mungu:

i. Mungu huendelea kufanya ulimwengu uendelea jinsi anavyotaka mwenyewe. Hii inaonyesha kwamba Mungu hategemei chochote, lakini mwanadamu anamtegemea Mungu. (Zaburi 63:8).

ii. Mungu husababisha kiumbe kienende na kufanya kulingana na mapenzi yake. Kiumbe na mwanadamu hawajitegemei bali wanategemea Mungu hata wakati wanaonekana kufanya kinyume na Mungu. Hii haimaanisha kwamba Mungu huhusika katika dhambi au ndiye mwanzilishi wa dhambi. Mwanadamu anaweza kuchanguwa kufanya mazuri au mabaya (Kumbukumbu la Torati 30:19). Lakini ukweli ni kwamba kila wakati mwanadamu anachagua kufanya mabaya (Mwanzo 6:5). Mwanadamu atachagua kufanya mazuri ikiwa ataongozwa na Mungu (Warumi 6:1,11,22).

a. Mungu huwa anadhibiti dhambi za wanadamu (Mwanzo 45:5 na 50:20).

b. Mungu huzuia mwanadamu asifanye dhambi kiwango ya kupindukia (Ayubu 1:12). c. Mungu hubadilisha ubaya na kufanya mazuri (Mwanzo 50:20).

iii. Mungu ndiye anaendelea kutawala kila kitu ili kila kitu kifanyaika kwa mapenzi na kusudi lake. Katika Biblia mara kwa mara Mungu anafundisha kwamba Yeye ndiye mfalme wa ulimwengu na anatawala kila kitu kulingana na mapenzi yake (Zaburi 22:28 na Isaya 33:22).

VII. Mafundisho ya Biblia kumhusu mwanadamu na uhusiano wake na Mungu.

1. Hali ya mwanadamu.

A. Jinsi mwanadamu alivyo

i. Mwanadamu anajumlisha mwili na nafs (Mathayo 10:28 na 1 Wakorintho 5:3 na 5).

B. Mwanadamu ameumbwa katika mfano wa Mungu.

i. Mungu alimwumba mwanadamu kama kilele cha kazi yake ya uumbaji. Mwanadamu ndiye pelee aliumbwa katika mfano wa Mungu (Mwanzo 1:26-27).

C. Je, kuumbwa katika mfano wa Mungu inamaanisha nini?

i. Mwanadamu ni kiumbe cha kiroho, mantiki, maadili, asiyekufa milele. Yeye anaweza kuwa na uhusiano na Mungu. Ndani mwake Mungu na kazi zake zina dhihirika. Viumbe vingine haviko hivi (Mwanzo 9:6 na Yakobo 3:9).

A. Mungu alitengeneza makubaliano na mwanadamu ambapo anamwagiza mwanadamu aweze kumtii (Mwanzo 2:16-17). Ikiwa mwanadamu atatii Mungu, yeye atapata uzima wa milele (Warumi 10:5; Wagalatia 3:12).

3. Mambo yaliomo katika Agano la matendo.

A. Mungu alimpa mwanadmu Baraka za uzima wa milele na furaha kamili. Hii ilihitajika kwamba mwanadamu angemtii Mungu kabisa.

B. Ahadi ya Agano ilikuwa uzima wa milele katika utakatifu kamili.

C. Agano hili lilikuwa liendelee kama mwanadamu angeendelea kutii.

D. Madhara ya kutotii yalikuwa ya kimwili, kiroho na hukumu wa milele. Hukumu ni kutenganishwa na Mungu milele.

4. Hali ya agano hili leo

A. Hata leo Mungu bado anawaamuru wanadamu waishi maisha matakatifu (Walawi 18:5 na Wagalatia 3:12). Lakini tunapaswa kufahamu kwamba baada ya kuanguka katika dhambi, hakuna mtu leo ambaye ana uwezo wa kutii kikamilifu.

B. Yesu Kristo pekee ndiye alitii kabisa. Kupitia kwake, tunaweza kupata uzima wa milele na kuhesabiwa watakatifu kabisa. Kupitia kwa kutii kwa Kristo kabisa, tunapata uzima wa milele (Waebrania 11:6).

5. Mwanadamu katika hali ya dhambi.

A. Mwanzo wa dhambi wakati mwanadamu alipoanguka katika dhambi. Biblia ianfundisha kwamba chanzo cha uovu ni dhambi ya Adamu (Mwanzo 3:6).

B. Hali ya dhambi ya kwanza ili kukosa kumtii Mungu. Dhambi yenyewe ilikuwa kukula tunda ambalo Mungu alikuwa amekataza Adamu kula. Cha muhimu hapa ni kwamba Adamu alikosa kumtii Mungu. Adamu alikataa Mungu asiongoze maisha yake. Hiki kilikuwa kitendo cha kiburi na mwanadamu kutaka kuwa kama Mungu.

C. Tunajua kwamba ni shetani ambaye aliwajaribu. Shetani alimtumia nyoka kuwajaribu kuanguka katika dhambi. Leo kuna wengi ambao wanatumiwa na shetani kuwajaribu watu wa Mungu kuanguka katika dhambi. Kwa ambao tumeokoka, tunapaswa kuhakikisha kwamba hatutumiwa na shetani.

D. Matokeo ya dhambi ya kwanza. Kila kitu kibaya katika ulimwengu kilianza. Mwanadamu alipoteza ufahamu wa kweli kumhusu Mungu. Mwanadamu alianguka kabisa katika dhambi na akawa mbaya sana na kuwa na uwezo wa kufanya mabaya.

6. Jinsi dhambi ilivyo.

A. Dhambi ni chochote ambacho tunakifanya, kuongea na kuwaza ambacho ni kinyume na Mungu (Mwanzo 2:17-18). Kwa sababu hii, huwa tunafanya dhambi kupitia kwa matendo na pia tunafanya dhambi bila kutenda.

B. Luka 11:23, tunasoma kwamba hakuna kuwa katikati, unaweza kuwa tu upande wa Mungu au upande wa shetani.

C. Kila mwanadamu anazaliwa akiwa na hali ya dhambi (Yeremia 17:9).

D. Dhambi inatufanya tuwe na hatia mbele za Mungu (Warumi 1:18; 3:23 na 6:23).

E. Dhambi imo ulimwenguni kote (1 Wafalme 8:46). Kila mtu ni mwenye dhambi

VIII. Mwanadamu na Agano la neema au ukombozi.

1. Neno Agano linamaanisha makubaliano kati ya pande mbili. Mungu alifanya makubaliana na wanadamu mara kwa mara.

2. Ninataka tuone Agano mbili ambazo mara kwa mara zimekosa kueleweka na wengine. Hizi ni Agano la Neema na la Ukombozi.

A. Agano la Ukombozi linatufundisha kwamba ukombozi wetu haikuwa mpango wa pili wa Mungu baada ya kuona Adamu na Hawa wameanguka katika dhambi. Linatufundisha kwamba Ukombozi ulikuwa mpango wa Mungu tangu mwanzoni (Waefeso 1:4;3:11; 2Timotheo 1:9, Yohana 5:30; 43; 6:38-40; 17:4-12).

i. Agano hili ni makubaliano kati ya Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Mwanadamu haumo katika Agano hili.

ii Katika Agano la ukombozi, Baba alimtuma Mwana aje katika mwili wa mwanadamu na aishi maisha matakatifu (Wagalatia 4:4; Waebrania 4:15). Mungu Baba alikuwa kamwe pamoja na Mwana katika kazi yake ya ukombozi.

iii. Mungu Mwana alikuwa alipe deni la dhambi zetu ili tuweze kupata uzima wa milele (Yohana 10:11 na Wagalatia 1:4).
iv. Agano hili halihitaji sisi tujitahidi kwa njia yoyote, isipokuwa tu kutii. Hii inamaanisha kwamba tunapaswa tu kukubali ahadi za agano hili kwa Imani (Waefeso 2:8).

v. Mungu aliahidi kwamba angemtuma Roho Mtakatifu aje:

a. Awalete na kuwaza watu wake mara ya pili na kuwaongoza katika utakatifu. Roho Mtakatif anaongoza, analinda na kulifundisha kanisa la Mungu (Yohana 14:26; 15:26; 16:13, 14).

b. Roho anahakikisha kwamba Kristo anawapokea watu wake wote ambao alipewa na Mungu Baba (Yohana 6:37, 39, 40, 44, 45).

c. Hawa watu ambao Kristo angepewa wao ni baadhi ya Ufalme wake (Zaburi 22:27; 72:17).

B. Agano la Neema. Agano hili linauhusiano wa karibu na Agano la Ukombozi. Huwa linafafanuliwa kuwa makubaliano ya neema kati ya Mungu na mwenye ambaye ameteuliwa, ambapo Mungu anamptaia Baraka mwenye dhambi. Mwenye dhambi anamkubali Mungu na Baraka zake kwake kwa Imani (Kumbukumbu la Torati 7:9; 2 Mambo ya nyakati 6:14; Zaburi 25:10, 14; 103:17, 18),

i. Ahadi na matarajioa ya agano la Neema.

a. Mungu aliahidi kwamba yeye atakuwa Mungu wetu nasi tutakuwa watu wake katika maisha ambayo hayaishi (Yeremia 31:33, Tito 3:7; Waebrania 11:7 na Yakobo 2:5).

b. Tunatakikina kukubali agano hili kwa Imani na kujitolea kwa Mungu katika utiifu.

ii. Hali ya Agano hili.

a. Agano hili ni la milele (Waebrania 13:20).

b. Agano hili linafanya kazi kwa wale tu ambao wameokoka, Wayahudi na Wayunani.

c. Agano hili ni sawa katika Agano la kale na Jipya (Mwanzo 3:15; Wagalatia 3:8). Katika Agano hizi, mwakilishi ni Kristo (Waebarnia 13:8; Matendo 4:12).

IX. Mafundisho kuhusu Kristo Yesu na Kazi yake.

1. Majina ya Kristo Yesu.

A. Haya ni majina muhimu ya Kristo.

i. Jina Yesu ni sawa na Yoshua (Yoshua 1:1; Zekaria 3:1; Ezra 2:2). Jina Yesu kwa kiebrania linamaanisha mwokozi (Mathayo 1:21).
ii. Kristo katika Agano la kale ni Mesiya, ambalo linamaanisha aliyepakwa mafuta (matendo 4:27; 10:38). Yesu ndiye aliitwa mpakwa mafuta.

iii. Mwana wa Adamu. Jina hili la Kristo linapatikana haswa katika Kitabu cha Danieli 7:13. Linadhihirisha kwamba Yesu ni Mwandamu ambaye atakuja juu ya miwangu katika utukufu (Mathayo 16:27, 28, 64, Luka 21; 27).

iv. Mwana wa Mungu. Yesu ni mwana wa Mungu kwa sababu Yeye ni wa pili katika Utatu wa Mungu. Pia Yeye mwenyewe ni Mungu. Yeye alizaliwa kwa nguvu za Roho Mtakatifu (Luka 1:35 na Mathayo 11:27).

v. Bwana Yesu Kristo. Jina ambalo linadhihirisha kwamba Kristo anamiliki na anatawala kanisa (Warumi 1:7 na Waefeso 1:17).

2. Jinsi Kristo alivyo. Biblia inatufundisha Kristo kwamba yeye ana hali mbili: Yeye ni mwanadamu na pia Yeye ni Mungu (Mathayo 16:16 na Yohana 1:1).

A. Yesu wa Nazareti ni Mungu ambaye alichukua mwili wa mwandamu. Hii inamaanisha kwamba Yeye alikuwepo hata kabla ya kuja humu ulimwenguni (Yohana 1:1). Katika kuwa kwake mwanadamu, tunaona kwamba ilikuwa hali ya kujinyenyekeza. Yeye hakuona kama kitu hata kama Yeye alikuwa alikuwa Mungu ambaye ameumba na kutawala kila kitu alichukuwa

mwili wa mwanadamu na akawa mtumishi (Yohana 1:14; 1 Yohana 4:2). Kwa ufupi ni kwamba kila wakati Yesu amekuwa Mungu, na ile aweze kutokoka, aliacha utajiri wa mbinguni na akawa mwanadamu na kuishi miongoni mwetu.

B. Lakini hata alijinyenyekeza, Kristo bado aliinuliwa. Yeye aliinuliwa kwa njia kwamba hata baada ya kufa, alifufuliwa kutoka kwa wafu na akapa na kurudi mbinguni. Sasa ameketi mkono wa kuume wa Mungu na atarudi katika utukufu kuhukumu ulimwengu siku ya mwisho (1 wakorintho 15:4, marko 16:19 na Matendo 17:31).

C. Yesu ni mwanadamu pia. Katika Yesu Kristo, tunaona Mungu katika mwili wa mwanadamu (1 Timotheo 3:16; Yohana 8:20 na Matendo 2:22, Warumi 5:15). Kama mwanadamu, yesu aliyapitia yote ambayo tunayapitia kama wanadamu kama majaribu, njaa huzuni na kadhalika. Lakini katika haya yote, Yeye hakufanya dhambi.

D. Hali hizi mbili za Kristo zimeungana katika Kristo. Hii inamaanisha kwamba Kristo ni mwanadamu na Yeye ni Mungu. Huwezi ukatenganisha hali mbili za Kristo.
i. Yeye ni Mungu na Yeye ni mwandamu. Ukweli ni kwamba hatuelewi kabisa jambo hili lakini kwa sababu Biblia inalieleza, tunapaswa kuliamini (Yohana 10:30, 17:5).

3. Uhusiano kati ya Yesu na sheria.

A. Kuneyenyekea kwa Kristo kunamaanisha kwamba, hata kama yesu alikuwa Mungu, hakuona kama ni kitu cha kukwamilia, bali alichukua alifanyika mwanadamu ili aweze kuwa mtumwa. Kwa ufupi ni kwamba, Yesu ambaye ni Mungu mwenye kupeana sharia, alijiweka chini ya sheria mwenyewe alipofanyika mwandamu.
i. Yesu alipofanyika mwadamu na kuzaliwa kwake. Yesu alizaliwa na Maria ambaye alikuwa mwandamu. Kwa sababu hii Yeye ni mwanadamu (Isaya 7:14 na Mathayo 1:20-21). Yeye alizaliwa kwa nguvu za Roho Mtakatifu. Yeye ndiye pekee katika kizazi cha wanadamu kuzaliwa na bikira. Hii inamaanisha kwamba Yesu hakuzaliwa akiwa mwenye dhambi kama wanadamu wengine (Luka 1:34-38).

ii. Kristo katika maisha yake yote, alikuwa mtu wa mateso. Yeye alikaliwa na kuumizwa na maadui wake. Yeye pia alijaribiwa na shetani, na kunyanyaswa na dhambi za walimwengu. Yeye alizibeba dhambi za walimwengu (Isaya 53:3).

iii. Kifo cha Yesu kilikuwa kifo cha kimwli ambacho kilifanyika kwa sababu ya kuzib eba dhambi zetu (Isaya 53:12). Kifo chake msalabani kilikuwa kifo cha laana (Kumbukumbu la Torati 21:23 na Wagalatia 3:13).

iv. Kuzikwa kwa Kristo pia kulikuwa njia ya unyenyekevu wake kwa sababu ndio njia ya mwandamu ya kurudi mavumbini kama matokeo ta laani (Mwanzo 3:19).

B. Kufufuka kwa Kristo Yesu kunadhihirishi kwamba Yeye alikuwa ameshinda dhambi. Yeye alifufuka na kurudi mbinguni mahali ambapo ametunukiwa tajin a heshima. Yeye aliregeshima utukufu na heshima ambavyo vilikuwa vyake tangu hapo mbeleni.

C. Kuna hatua nne za kutukuzwa kwa Kristo:

i. Kufufuliwa ilikuwa hatua ya kwanza. Hii inamaanisha kwamba Kristo alipewa uhai wake kama wamdamu tena. Mwili wake na nafsi ziliregeshewa uzuri wake wa kwanza. Yeye alifufuka akiwa na mwili mpya (1 wakorintho 15:44-45). Hii ndio sababu anaitwa mzaliwa wa kwanza miongoni mwa wale ambao wamekufa (1 Wakorintho 15:20). Kupitia kwa kufufuka kwake, Yeye alifanyika nafsi ambayo inapeana uzima (1 wakorintho 15:45). Kufufuka kwa Kristo ni muujiza ambayo ni knyume cha hali ya maisha. Ni lazima sisi sote tuamini jambo hili. Kufufuka kwa Kristo kunaashiria mambo matatu muhimu:

a. Kunadhirisha kwamba Mungu Baba alitosheka kwamba sharia yake takatifu ilitekelzwa kikamilifu.

b. Inaonyesha kile ambacho kitawafanyikia wale ambao wameokoka (Warumi 6:4-5; 1 Wathesalonike 4:14).

c. Kwa sababu ya kuufuka kwa Yesu, sisi tunahesabiwa haki, tunazaliwa mara ya pili na tutafufuliwa (Warumi 4:25 na 1 Petro 1:3).

ii. Hatua ya pili ya kutukuzwa kwa Yesu ni wakati alipopaa na kurudi mbinguni akiwa mshindi. Hatua hii inakamilisha kufufuka kwa Yesu. Hii ni ishara ya kuhakikishiwa kwetu nafasi mbinguni (Waefeso 2:6).

a. Alipopaa, aliketi mkono wa kuume wa Mungu Baba. Hii ni nafasi ya mamlaka na utukufu (Waefeso 1:20 na Waebrania 10:12).

iii. Kuketi mkono wa kuume wa Mungu ni kuoneysha kwamba Yesu yupo katika nafasi ya mamlaka na utukufu. Yeye anatawala na kulinda kanisa lake. Yeye anatawala ulimwengu wote na anaendelea kuwaombea watu wake.

iv. Kutukuzwa kwa Kristo kutafika kilele atakaporudi kuwahukumu waliohai na wafu (Matendo 1:11 na Ufunuo 1:7).

_____-

Kwa ufupi:

1. Kunyenyekezwa kwa Kristo kunapatikana katika Wagalatia 3:13; 4:4-5; Wafilipi 2:6-8).

2. Yesu alikuja katika mwili wa mwanadamu (Yohana 1:14 Warumi 8:3).

3. Yesu alizaliwa na bikira (Isaya 7:14 na Luka 1:35).

4. Kufufuka kwa Kristo (Warumi 4:25 na 1 Wakorintho 15:20).

5. Yesu alipaa mbinguni (Luka 24:51 na Matendo 1:11).

6. Yesu atarudi (Matendo 1:11 na Ufunuo 1:7).

---

4. Kazi ya Kristo

A. Afisi za Kristo. Yesu ana afisi tatu kulingana na Biblia; Yeye ni nabii, Yeye ni kuhani na Yeye ni Mfalme.

i. Agano lilitabiri kuhusu kuja kwake kama nabii (Kumbukumbu la Torati 18:15; Matendo 3:22-23).

a. Yesu alijizungumzia Yeye kuwa ni nabii (Luka 13:33).

b. Yesu alieleza kuhusu mambo ya mbeleni (Mathayo 24:3-35, Luka 19:41-44).

B. Agano la Kale pia lilitabiri kuja kwake akiwa kuhani (Zaburi 110:4; Zekaria 6:13).

i. Yeye ni kuhani mkuu (Waebrania 3:1; 4:14; 5:5; 6:20; 7:26; 8:1).

ii. Yeye ni kuhani ambaye anaondoa dhambi (Yohana 1:29; Warumi 3:24).

iii. Kazi ya Yesu akiwa Kuhani mkuu ilikuwa kwanza, kuleta dhabihu kwa ajili ya dhambi. Dhabihu za Agano la kale zilikuwa zinatuelekeza kwa dhabihu kuu ya Yesu (Waebrania 9:24; 13:11-12).

a. Akiwa dhabihu, aliitwa mwana-kondoo wa Mungu (Yohana 1:29).

b. Akiwa dhambihu pia anaitwa pasaka (1 Wakorintho 5:7).

c. Yesu akiwa kuhani mkuu wetu, Yeye hutuombea. Yesu mwakilishi na mwombezi wetu ambaye anaomba kwa niba yetu (1 Yohana 2:2 na Warumi 8:34).

d. Hii inamaanisha kwamba Yesu alijipeana kama sadaka kwa Mungu na kuchukua Baraka zote kwa ajili ya watu wake (Yohana 17:9,20).

C. Agano la Kale lilitabiri kuja kwa Kristo akiwa mfalme.

i. Yeye ni mfalme wa kiroho juu ya kanisa lake (Mika 5:2, Zekaria 6:13, Luka 1:33 na Yohana 18:36).

ii. Yeye pia ni mfalme wa ulimwengu wote (Mathayo 28:18).

a. Yeye ni mwakilishi wa kanisa lake. Yeye ni mfalme ambaye anatawala mataifa na maisha yetu. Yeye anatawala maisha ya watu wa ulimwengu na kuyafanya yaenende kulingana na kusudi lake la wokovu na kulinda kanisa lake dhidhi ya hatari ya ulimwengu. Ufalme wa hapa dunia utaendelea hadi wakati maduia wake watashindwa kabisa.
b. Wakati huu, ufalme wote utaregeshewa Mungu Baba (1 Wakorintho 15:24-28).

5. Katika upatisho ya Kristo Yesu. Kabla ya kuokoka, tuilikuwa maadui wa Mungu. Kazi ya upatanisho ya Kristo inatuwezesha kuwa na Amani na Mungu. Tumepatanishwa na Mungu na hasira yake dhidi yetu kuondolewa kupitia sadaka ya kifo cha Yesu.

A. Kile kilicho sababisha na umuhimu wa kazi ya Kristo ya upatanisho.

i. Hili ndilo Kusudi la Mungu (Isaya 53:10, Waefeso 1:6-9).

ii. Hii ilikuwa kudhihirisha upendo wa Mungu (Yohana 3:16)

iii.Biblia ianasema kwamba Mungu mwenye haki na Mtakatifu hawezi kamwe kupuuza dhambi, Yeye ni lazima aiadhibu dhambi (Kutoka 20:5 na Warumi 1:18).

iv. Mungu alikuwa ameamua kuwahukumia kifo wenye dhambi wote I(Mwanzo 3:3, warumi 6:23). Njia moja tu ambayo Mungu angeweza kutusamehe ilikuwa kupitia kwa kifo cha Kristo ambaye hakuwa na dhambi.

B. Hali ya kazi ya upatanisho au kifo cha Kristo:

i. Kifo cha Yesu kilitosheleza haki ya Mungu. Kazi kuu ya kifo cha Yesu ilikuwa kutupatanisha Mungu na mwenye dhambi. Kazi ya pili ilikuwa kupatanisha mwenye dhambi na Mungu.

ii. Yesu alipokufa alichukua nafasi yetu. Mungu alikubali kifo cha kristo kwa niaba yetu. Kwaq ufupi ni kwamba kifo cha Yesu kilikuwa kifo chetu. Lakini Kristo aliamua kufa kwa niaba yetu ili sisi tupata kusamehewa tunapomwamini.

a. Agano la Kale linafundisha wazi kabisa kuhusu kifo cha Yesu Kristo. Ni lazima damu ingemwagika (Walawi 1:4; 17:11).

b. Biblia ianfundisha kwamba dhambi zetu ziliwekwa juu ya Kristo (Isaya 53:6).

c. Kristo alilipa deni la dhambi zetu (Yohana 1:29) na aliyatoa maisha yake kwa ajili yetu (Wagalatia 1:4)

C. Kazi ya upatanisho ilihusu kufanya mambo fulani na utiifu. Mambo haya mawili hayawezi kutenganishwa.

i. Yesu alitii sharia yote kwa niaba yetu ili tuweze kupata uzima wa milele. Mfano wa utiifu wake ni:

a. Yesu alitii sharia ya Mungu kikamilifu ili tupate uzima wa milele.

b. Yesu lijitoa ili ateseke na kufa kwa ajili yetu (Yohana 10:18).

ii. Kuna mambo mengine ambayo Yesu Kristo aliyapitia kwa ajili ya kutuokoa. Kwa mfano:

a. Kuna mateso mengi ambayo aliyakubali kama njia ya kulipa deni la dhambi zetu.

b. Yeye aliiti sharia bila mabishano.

iii. Aina hii ya mateso hatuwezi kutenganisha.

iv. Kupitia kwa utiifu wake, Yesu alilipia deni la dhambi na kundoa madhara ya laana kwa wale ambao wanamwamini (Isaya 53:6 na Warumi 4:25).

v. Pia kupitia kwa utiifu wake alitununulia uzima wa milele wale ambao wanamwamini (Mwanzo 4:4-5).

D. Hata kama kifo cha Yesu kinauwezo wa kuwaokoak wote, si wote wataokoka. Ukweli ni kwamba si kila mtu kwamba ataenda mbinguni.

i. Kristo aliyatoa maisha yake kwa ajili ya watu wake (Mathayo 1:21).

ii. Yesu alikufa kwa ajili ya kondoo wake (Yohana 10:11).

iii. Yesu alikufa kwa ajili ya kanisa lake (matendo 20:28).

X. Mafundisho kuhusu kazi ya Roho Mtakatifu.

1. Roho Matakatifu pia hufanya katika maisha ya watu wote hata wale ambao hawajaokoka.

A. Yeye anafanya kazi kwa njia ambayo anawazuia watu wasitende dhambi jinsi wangeweza kutenda.

B. Kuna neema ya kawaida kwa kila mtu ambapo Mungu anapeana bila kubagua. Hata kama kifo cha Yesu hakitamwokoa kila mtu, ulikuwa ni hata wale ambao hawajaokoka, wanafaidika kutokana na kifo hicho. Maisha yangekuwa mabaya sana hapa ulimwenguni kama hakungekuwa na neema ya kawaida kwa kila mtu. Kwa mfano:

i. Maisha yetu yanaendelea kwa sababu ya neema ya kawaida. Mungu hamhukumu mtu kwa haraka kwa sababu Mungu anampatia mtu muda wa kutubu (2 Petro 3:9).

ii. Kupitia kwa neema ya kawaida, Mungu anazuia uovu mwingi sana. Mungu anafanya hivi wakati mwingi kupitia kwa sharia za wanadamu, mazungumzo ya wanadamu (Mwanzo 20:6, Ayubu 2:6).

iii. kila mwanadamu ana hisia za tabia nzuri na mbaya, ukweli na uongo. Kila mwanadamu ana tamaa ya ukweli, uzuri na urembo (Warumi 2:14-15 na Matendo 27:22).

iv. Kwa sababu ya neema ya kawaida, watau hata wale ambao hawajaokoka wanaweza kufanya mambo mazuri (2 Wafalme 1:29-30 na Luka 6:33).

v. Neema ya kawaida inaonekana hata wakati Mungu anafnya nvua inyeshe na mimea ikue. Wanadamu wote wanapata Baraka nyingi sana ambazo hawastahili kutoka kwa Mungu (ZAburi 145:9, Matendo 14:16-17).

XI. Kuitwa na kuzaliwa mara ya pili. Maana ya kuitwa ni mwaliko ambao tunausikia kutoka kwa mahubiri.

1. Mungu huwaita wenye dhambi kupitia kwa mahubiri ya neno lake ili wapate kumwamini Kristo (1 Wakorintho 1:9).

A. Kuitwa kwa nje ni mahubiri amabyo inawalika wenye dhambi ili mwamini Kristo. Wakati huo wenye dhambi wakihimizwa kumkubali Kristo kwa Imani ili wapate msamaha wa dhambi na uzima wa milele. Mwito huu unajumlisha:

i. Kueleza ukweli wa ujumbe wa injili (Mathayo 28:19).

ii. Mwaliko kwa ajili ya kutubu na kumwamini Kristo (Marko 1:15).

iii. Ahadi ya msamaha na wokovu (Luka 1:77).
iv. Mwito huu unahitaji Imani ya kweliu na toba. Huu ni mwito wa kweli kutoka kwa Mungu ambaye ni mwaminifu (Hesabu 23:19).

v.Mwito wa Mungu kupitia kwa mahubiri ya injili ni kwa watu wote (Isaya 45:22).

vi. Ikiwa Mtu anakata kutii mwito wa Mungu kwake hata baada ya kuusikia, ni wazi kwamba hukumu yake ni kubwa hata kuliko yule ambaye hajawahi kusikia. Hii ni kwa sababu yule ambaye amesikia ana nafasi ya kuamini lakini anakataa (Yohana 5:39-40).

B. Mwito wa ndani ni kazi ya Roho Mtakatifu ndani yam yoyo wa mwanadamu.

i. Mwito unatokana na neno la Mungu wakati Roho Mtakatifu analichukua na kulifanya liwe hai katika mwoyo wa msikilizaji (1 Wakorintho 1:23-24).

ii. Huu ni mwito wa nguvu sana kwa ajili ya wokovu (Matendo 13:48).

iii. Mwito huu hauwezi kupingwa au kukataliwa au kuondolewa (Warumi 11:29).

2. Kuzaliwa mara ya pili

A. Kuzaliwa ya pili ni jambo la muhimu kwa mtu yeyote kuokoka. Yesu alimwambia Nikodemo kwamba alihitaji kuzaliwa mara pili. Yaani alihitaji kuzaliwa kiroho (Yohana 3:7). Wale wote ambao wameokoka, wamezaliwa mara ya pili.

B. Kuzaliwa mara ya kwanza ndio hatua ya kwanza katika wokovu. Hapa ndipo kazi ya neema inaanza katika m moyo wa mwenye dhambi. Huu ndipo wakati Mungu anapeana moyo mpya (Ezekieli 36:26-27).

C. Kuzaliwa mara ya pili, inatuongoza kwa hatua ya pili ambayo ni toba na imani.

XII. Kuokoka, ni toba na Imani au kumgeuka kutoka kwa dhambi na kumgeukia Mungu.

1. Imani ya kweli huongoza kwa kutubu ambako ni kugeuka kutoka kwa dhambi na kumgeukia Mungu (Matendo 3:19). Kutubu kwa kweli kunahitaji kugeuka kutoka kwa dhambi na kumgeukia Mungu.

A. Kutubu kwa kweli kunahitaji mtu aelewe kwamba dhambi ni uasi dhidi ya Mungu. Halafu mtu huyu kwa kweli anamua kuacha dhambi na kuishi maisha ya kumpendeza Mungu ambayo msingio wake ni Imani ndani ya Kristo (Matendo 26:20).

B. Imani ya kweli msingi wake ni Kristo ambaye alifidia dhambi zetu. Kumwamini Kristo ni kusamehewa dhambi (matendo 20:21, Warumi 3:25).

i. Imani ya kweli inazaa matendo ya Imani katika maisha ya mtu ambaye anaamini injili. Imani ya kweli inaonekana katika matendo.

C. Imani ambayo inaokoka inaleta mabadiliko ambayo inaoingoza mtu katika upatanisho na wokovu. Mabadiliko haya ni:

i. Toba: Mtu anatubu dhambi zake. Biblia inazungumza kuhusu Imani hii mara 65 (Matendo 2:38, Mathayo 3:2. Marko 1:15, Luka 13:3). Kutubu inamaanisha kukiri dhambi na kwamba wewe kweli unahuzunika kwa ajili ya dhambi na kuomba Mungu akusamehe dhambi zako. Pia unapaswa kumwomba Mungu akusaidie ili uache kuendelea katika dhambi. Toba lazima itoke kwa moyo na wala si maneno matupu tu.

ii. Kupenda Mungu ni kutii kile ambacho Mungu anasema (Yohana 3:36, Luka 6:46, 1 Yohana 2:3-4). Biblia inasema kwa hili tunajua kwamba tumemjua, ikiwa tunatii amri zake. Yeyote anasema kwamba anamjua Munngu, lakini hatii amri za Mungu, yeye ni mwongo na ukweli haumo ndani mwake. Ni lazima tumtii Mungu.

iii. Tuwe na tamaa ya kufanya kazi ambazo zinampendeza Mungu (Wagalatia 5:13, Luka 14:26, 2 Wakorintho 8:5, 1 Petro 4:10, Warumi 12:11). Tusikate tamaa, lakini tujwe na ukakamavu katika kiroho, na tumtumikie Mungu. Mtumikie Mungu kwa moyo wako wote.

D. Toba haliishi baada ya sisi kuokoka. Ukweli ni kwamba hata baada ya kuokoka, huwa tunatenda dhambi mara kwa mara (Zaburi 51).

XIII. Upatanisho na ukombozi

1. Upatanisho ni kuondoa uadui ambao umeletwa na dhambi. Inamaanisha kumaliza vita kati ya mwenye dhambi na Mungu, na kuleta Amani na Mungu (Warumi 5:10, Waefeso 2:16).

A.Kuna hatua nne ambazo zinapatikana katika upatanisho (2 Waqkorintho 5:18-21).

i. Mungu huwa hatuhesabii dhambi baada ya kutuokoa. Mtu ambaye ameokoka, hatawahi kuadhibiwa kwa sababu ya dhambi zake, kwa sababu Yesu amesha adhibiwa kwa niaba yetu.
iv. Mungu anapotuokoa, Yeye hutupatia haki ya Kristo kuonyesha kwamba ametupatisha Naye. Yeye hutuondolea hatia.

2. Kukombolewa inamaanisha kuwekwa huru kutoka katika utumwa wa dhambi kupitia kwa kifo cha Kristo Yesu msalabani. Kabla ya kukombolewa, tulikuwa watumwa wa dhambi. Lakini baada ya kukombolewa, tumepata Bwana mwingine ambaye ni Kristo.

A. Utumwa kwa dhambi ni jambo la ukweli. Katika historia tuna mifano ya wengi ambao wanaishi katika dhambi na wanaendelea katika dhambi (Genesis 3-4). Kuna mafundishi mengi katika Agano la kale na Jipya kuhusu dhambi ambayo imewafanya wanadamu kuwa watumwa.

i. Kila wazo la mwanadamu liliongozwa na dhambi (Mwanzo 6:5).

ii. Kilele cha dhambi ni wakati wanadamu walipomwua Yesu msalabani kalivari.

iii. It is from our bondage to sin that Jesus came to redeem us.

B. Mkombozi ni Yesu ambaye alilipa gharama ambayo ilitukomboa kutoka kwa utumwa wa dhambi. Yesu anatukomboa kutoka kwa:

i. Uovu wote (Tito 2:14).

ii. Utumwa wa dhambi (Warumi 6:18,22)

iii. Laana ya sharia (Wagalatia 3:13)

iv. Utumwa wa sharia (Wagalatia 4:5)

v. Kifo (Ayubu 5:20).

vi. Jahanum (Zaburi 49:15).

3. Kukomboa inamanisha kukunua mtu kutoka kwa utumwa. Lakini gharama ya ukombozi ilikuwa kubwa sanna.

A. Gharama ya ukombozi wetu ilikuwa damu ya Yesu (1 Petro 1:18-19).

B. Sababu ya Yesu kuja katika ulimwengu ilikuwa ni kutukomboa (Marko 10:45).

C. Sheria ilihitaji tuhukumiwwe milele (Warumi 6:23). Sheria ya Mungu, na haki yake vilitoshelezwa na sadaka ya Kristo Yesu. Mungu alikubali na kutosheka na sadaka ya Yesu (Wagalatia 3:13). Kwa ufupi ni kwamba Yesu alidhibiwa kwa ajili ya dhambi zetu ili sisi tuweze kusamehewa na tuweze kuingia mbinguni na wala si jahanum.
4. Tuliumbwa ili tuwe na uhusiano na ushirika mwema na Mungu. Lakini kupitia kwa dhambi yetu, uhusiano na ushirika huu ulivunjika. Yesu alitupenda sana kiwango kwamba alitukomboa kwa damu yake. Yeye aliondoa hatia yetu ya dhambi na kutuvisha haki yake.

XIV. Kufanya mweny haki. Kufanywa mwenye haki ni hali ya sharia ambapo mwenye dhambi anataganzwa huru kwa sababu ya haki ya Kristo. Kwa ufupi ni kwamba Mungu anamtanagaza mwenye dhambi huru, au anamwonodolea makosa yote. Kufanywa mwenye haki ni kinyume na kuhukumiwa.

1. Hali ya kufanywa mwenye haki (Warumi 3:21-26).

A. Mungu anamsamehe mwenye dhambi, dhambi zake zote, za jana, leo na za mbeleni. Ni kitendo cha mara moja (Isaya 44:22; Waebrania 10:14).

i. Hata kama tumesahewa dhambi kabisa, bado tunastahili kutubu na kuhakikisha kwamba tunatafuta kuhakikishiwa wokovu na masamaha wa dhambi za kila siku.

ii. Kufanywa wana wa Mungu. Matokeo ya kufanywa wenye haki ni kufanywa wana wa Mungu na kupewa kibali cha uzima wa milele na urithi wa mbinguni (Waefeso 1:5; 1 Petro 1:4).

a. Kufanywa wana wa Mungu ni mapenzi ya Mungu (Waefeso 1:4).

b. Kufanywa wana wa Mungu ni Baraka kutoka kwa Mungu ambayo inatufanya warithi na wanarithi pamoja na Kristo.

B. Kuwa mrksto ni zaida ya kujua mambo fulani ya kweli ya Biblia. Sisi ambao tumeokoka, tumeunganishwa kwa Kristo, na kwa sababu hiyo,

i. Tuna Baraka zote za kiroho (Waefeso 1:3).

ii. Tumechaguliwa (Waefeso 1:4)

iii. Tunaletwa karibu na Mungu (Waefeso 2:13).

iv. Tunaumbwa upya (Waefeso 2:10)

v. Tunapendwa na Mungu (Warumi 8:39)

vi. Tunafanywa kuwa watu moja (Wagalatia 3:28).

C. Mtu anaweza kuwa katika Adamu au katika Kristo. Tunaweza kuwa wana wa Mungu au wa shetani.

i. Kuwa katika Adamu inamaanisha kuwa katika hali ya dhambi hali ambayo tunazaliwa ndani. Katika hali hii:

a. Dhambi na kifo ndiyo vinatawala (Warumi 5:17).

b. Tunakuwa chini ya hukumu wa Mungu (Warumi 5:18).

c. Maish yetu huwa ni ya kutotii Mungu (Warumi 5:19).

ii. Kuwa ndani ya Kristo inamaanisha:

a. Tulisulibishwa na Kristo na mtu wa kale (dhambi) alikufa.

b. Sisi ambao tumeokoka si watumwa tena wa dhambi (Warumi 6:6).

c. Tumekufa kwa mambo ya dhambi (Warumi 6:12).

d. Dhambi haitaishi tena ndani mwetu (Warumi 6:12).

D. Ukweli hapa ni kwamba tutafanya dhambi, lakini hii si tabia yetu ya kila siku. Mara kwa mara mioyo yeti itakuwa inatoroka dhambi na kupendezwa kutii Mungu. Dhambi haitatawala wamaisha yetu tena.

XV. Utakaso: Hii ni kazi ya Roho Mtakatifu ambapo anaendelea kututakasa kutokana na uchafu wa dhambi. Huu ni wakati ambapo tunaendelea kushinda dhambi.

1. Kazi ya utakaso huanza mara tu tunahesabiwa haki na Mungu. Yaani wakati ambapo tunaokoka.

A. Hii kazi ambayo Roho Matakatif anafanya katika maisha yetu yote wakati tumko hapa ulimwenguni. Katika kazi hii, tunaendelea kufanana na Kristo (1 Wathesalonike 4:3-4).

B. Katika maisha haya, hatuwezi kamwe kuwa wakamilifu (1 Yohana 1:8).

C. Tunakamilika kabisa wakati tumekufa (Waebrania 12:23).

2. Utakazo ni kazi kubwa ambayo inaonekana katika maisha ya mtu ambaye ameokoka (Wakolosai 3:1-10).

A. Kazi ya kufanywa kuwa wenye haki, ni kazi ya Mungu

B.Kazi ya utakaso pia ni kazi ya Mungu, ambapo Mungu anatuhusisha pia. Huwa tunamtegemea Mungu katika kazi (Wafilipi 2:12-13).
C. Ni lazima tuhakikishe kwamba tunatekeleza majukumu yetu katika kazi ya utakaso. Ni lazima tupinge hali ya dhambi na tuenenda katika roho (Waefeso 4:20-32).

D. Kazi ya Utakaso huzaa matendo mema ambayo sima makamilifu, lakini yanafanywa kwa upendo wa Mungu na kwa Imani (Waebrania 11:6).

i. Matendo haya mazuri yanafanywa kulingana na mapenzi ya Mungu (Yakobo 2:8).

3. Ni wakristo pekee ambao wanaweza kufanya matendo mema ambayo yanampendeza Mungu. Matendo ya wale ambao hawajaokoka yanafanywa si kwa upendo na Imani. Matando haya hayafanywi kwa utukufu wa Mungu. Matendo mazuri ya wale ambao hawajaokoka, hayawezi kuwaokoka.

4. Mungu anaamuru wakristo tuyafanya matendo mema, kwa sababu yanadhihirisha Imani yetu katika Kristo (Yakobo 2:14,17-18). Kumbuka kwamba matendo mazuri hayamwokoi yeyote, lakini yanadhihirisha Imani yetu katika Kristo.

XVI. Kuvumilia kwa wakristo.

Hii kazi ya Roho Mtakatifu katika maisha ya wakristo ambapo ana hakikisha kwamba haturudi nyuma na kuacha kumwamini Kristo. Hii inamaanisha kwamba mtu ambaye ameokoka, ataendelea kuwa ameokoka milele na hatapoteza wokovu wake (Wafilipi 1:6).

1. Tunapookolewa, huwa tunaletwa katika jamii ya Mungu na kupewa Baraka zote za kuwa mwana wa Mungu. Sisi tunafanywa wraith pamoja na Kristo. Kuwa wana Mungu ni jambo la milele (Warumi 8:15-17).

2. Hakuna chochote ambacho kinaweza kututenganisha na upendo wa Mungu (Warumi 8:38-39).

XVII. Mafundisho ya Biblia kuhusu kanisa na njia za neema.

1. Kanisa la Kristo moja ndio mwili wa Kristo ulimwenguni kote. Si mjengo wa mikono ya wanadamu. Kila mtu ambaye ameokoka, ni mmoja wa kanisa la Kristo. Yesu ndiye kichwa cha kanisa (Waefeso 5:23; Wakolosai 1:18,24).

2. Neno kanisa pia linaamanisha kila kanisa kila mahali duniani. Ni kanisa ambalo linakutana mahali tofauti ulimwenguni (Warumi 16:5,23).

3. Kanisa pia ni mwili wa wakristo ambao wanakutana pamoja. Kanisa la kweli linafanya mambo matatu:

A. kanisa linahubiri neno la Mungu (1 Yohana 4:1-3, 2 Yohana 9). Tunapaswa kukumbuka kila wakati kuhubiri tu neno la Mungu.

B. Kanisa linabatiza wale ambao wameokoka na linashiriki meza ya Bwana (Mathayo 28:19, 1 wakorintho 11:23-30).

C. Kanisa linatekeleza nidhamu (Mathayo 18:18, 1 Wakorintho 1:1-5).

4. Biblia inafundisha kwamba kanisa:

A.Linapaswa kuwa na umoja (Yohana 17:21 na Waefeso 4:4-6).

B. Linapaswa kuwa takatifu (Kutoka 19:6 na 1 Petro 2:9).

C. Kanisa ni moja ulimwenguni kote na kila mkristo ni mshirika katika kanisa hili. Mbinguni hakutakuwa na madhehebu, isipokuwa wakristo pekee (Zaburi 2:8 na Ufunuo 7:9).

D. Kanisa linapaswa kuzingatia ukweli kila wakati (2 Timotheo 1:13 na Tito 2:1).

5. Serikali na kanisa.

A. Kristo ndiye kichwa cha kanisa na chanzo cha kila mamlaka (mathayo 23:10 na 1 Wakorintho 12:5-6).

B. Wachungaji na mashemanzi wao hutumika wakiwa chini ya mamlaka ya Kristo (matendo 14:23).

i. Wachungaji wanaongoza, wanahubiri na kufundisha (1 Timotheo 5:17).

C. Mamlaka ya kanisa ni ya kiroho kwa sababu Roho Mtakatifu ndiye ana patiana mamlaka haya (Matendo 20:28).

D. Mamlaka ya kanisa ni ya kiroho (2 wakorintho 10:4).

E. Mamlaka ya kanisa yanatekelezwa kwa njia tatu:

i. Kanisa lina mamlaka ya kufundisha. Kanisa linapaswa kulinda ukweli na kufundisha ukweli huo kwa uaminifu kwa kila kizazi na kuulinda kutokana na mamlaka ya giza (1 Timotheo 1:3-4, Tito 1:9-11).

a. Kanisa linapaswa kuhubiri neno bila kukata tamaa katika kila taifa (2 Wakorintho 5:20; 1 Timotheo 1:3-4).

ii. Kanisa lina mamlaka ya kujiongoza kwa kuhakikisha kwamba sharia ya Kristo zinatekelezwa (Matendo 20:>28). Kanisa lina mamlaka ya kuadhibu (1 Wakorintho 5:2,7,13), kwa wazi na katika siri (mathayo 18:15-18).

iii. Kanisa lina mamlaka na nguvu za kuwashugulikia maskini, wajane na mayatima (Yakobo 1:27; marko 14:7, matendo 11:29).

6. Njia za neema, neno la Mungu, ubatizo na meza ya Bwana.

A. Neno la Mungu ndio njia kuu ya neema.

i. Neno la Mungu na Roho. Roho Mtakatifu anafanya na neno la Mungu kwa kulifanya liwe hai na nguvu katika maisha yetu (1 Wakorintho 2:10-14).

B. Ubatizo na Meza ya Bwana.

i. Katika Agano la kale kulikuwa na kutahiriwa na pasaka. Yote ilihusu kumwaga damu.

ii. Agano Jipya lina Ubatiza na Meza ya Bwana, na hakuna damu ambayo inamwagwa. Baada ya sadaka ya Kristo Yesu, hakuna tena damu nyingine itamwagwa.

C. Yesu aliamuwa ubatizo ufanyike baada ya kufufuka (Mathayo 28:19. Kila mtu ambaye amkiri kuokoka ni lazima abatizwe (Matendo 2:38, 8:36).

D. Yesu alianzisha meza ya Bwana wakati wa pasaka kabla ya kifo chake. Mkate ni mfano wa mwili wa Kristo na kikombe ni mfano wa damu ya kristo. Meza ya bwana ni mfano wa kifo cha Kristo na inatukumbusha Baraka za kifo cha Kristo (1 Wakorintho 11:26).
i. Kusihiriki kwetu katika meza ya Bwana inadhihirisha kushiriki kwetu katika kifo cha Kristo na kushiriki kwetu katika maisha na nguvu za Bwana yesu.

E. Meza ya Bwana ni hakikisho la wokovu wetu kupitia kwa sadaka na kufufuka kwa Kristo.

F. Meza ya Bwana inapaswa kuliwa na wale tu ambao wameokoka kwa sababi ni wao tu ambao wanaelewa maana yake. Haifai kuliwa na watoto au mtu yeyote ambaye hajaokoka.

i. Hata wale ambao wameokoka, wanapaswa kujichunguza kwanza kabla ya kula (1 Wakorintho 11:28-32).

XVIII. Mafundisho kuhusu mambo ya mwisho.

1. Miili yetu itakufa, ikiwa hatutaishi hadi kristo kurudi (Mhubiri 3:1-2; 1 Wathesalonike 4:17). Kifo cah mwili tofauti kabisa na kufa kufa kwa nafsi (Mathayo 10:28). Nafis haikufi milele bali ikiwa mtu hajaokoka, nafsi itaenda jahanum, hiki ndicho kifo cha pili.

A. Mtu anapokufa, mwili na nafsi hutengamana (Mhubiri 12:7).

B. Kifo ndio mshara wa dhambi (Warumi 5:12).

2. Kurudi kwa Yesu kumetajwa mara 318 katika Agano Jipya. Kurudi huku kwa Yesu ni siri, kwa sababu hii hatufai kumwamini yeyote ambaye anasema kwamba anajua siku ya kurudi kwa Yesu (Marko 13:32).

A. Yesu atarudi kwa nguvu na mamlaka (Mathayo 24:30).

B. Yeye atarudi kutuleta katika uzima wa miledle. Yeye atafanya hivi kwa matyukio mawili: ufufuo na hukumu (1 Wathesalonike 4:13 na Ufunuo 22:12).

i. Bibli ianfunidsha kwamba Yesu atakaporudi wafu watafufuliwa na wale ambao watakuwa hai watakutana naye hewani (1 WEathesalonike 4:13).

ii. Miili ya wale ambao walikufa katika Kristo na wale ambao walikufa bili Kristo itafufuliwa (Danieli 12:2).

C. Kufufuka huku kutafanyika wakati Kristo atarudi na mara tu hukumu itafanyika (Yohana 5:25-29).

i. Hakuna mtu ambaye anajua ni siku gani mambya haya yatafanyika (Mathayo 24:36).

3. Hali ya mwanadamu baada ya kifo, na kabala ya kuumbwa kwa mbingu mpya, na kabal ya kupewa miili mpya na hukumu ya mwisho.

A. Miili yote inazikwa (Mwanzo 3:19).

B. Kuna mahali ambapo nafsi zote zinaenda kabla ya hukumu wa mwisho.

i. Nafsi za wale ambao waamini Kristo zinaingia katika utukufu wa Mungu (2 Wakorintho 5:8; Wafilipi 1:23).

ii. Nafsi ya mtu ambaye ahajaokoka mara tu anapokufa inaenda kuzimu (Luka 16:22-24).

4. Hukumu ya mwisho na hali ya mtu ya mwisho

A. Ni lazima kutakuwa na hukumu ya mwisho (Matendo 17:31).

i. Yesu ndiye hakimu wa mwisho (Yohana 5:27; Mathayo 13:41). Malaika na wakristo watahusika pia (1 Wakorintho 6:2-3).

ii. Kila mwanadamu atasimama katika hukumu (Ufunuo 20:10).

iii.Hukumu itafanyika mara tu ya ufufuo (Yohana 5:28-29).

iv.Hukumu ya Mungu itakuwa ile ambayo imeelzwa katika Biblia. Mungu atamzawadia kila mwanadmu kulingana na jinsi alivyoishi maisha yake. Wengine mbinguni na wengine jahanum. Kuna utofauti wa hukumu kwa wale ambaoi watakuwa jahanum. Pia kuna utofauti wa kuzawadiwa na wale ambao watakuwa mbinguni (Mathayo 11:22-24; Luka 12:47-48 na Yohana 14:2).

B. Hali ya mwisho ya watu.

i. Hali ya mwisho ya wale ambao hawajaokoka.

a. Watapekelwa jahanum mahali pa mateso (Mathayo 13:42; Ufunuo 20:14-15).

b. Watateseka na kuingi katika mateso mara tu wanapokufa (Luka 16:23-24,28).

c. Hukumu yao ni ya milele (mathayo 25:46, marko 9:48).

d. Hawatahi kutokam jahanum na kuingia mbinguni (Luka 16:26).

ii. Hali ya mwisho ya wale ambao wameokoka.

a. Kiumb e kipya kitaanzishwa. Mbingu mpya nan chi mpya zitaumbwa (Zaburi 102:26-27; Ufunuo 21:1).

b. Mbinguni ni ya milele (Luka 1:33; Warumi 2:7).

c. Zawadi ya wale ambao wamekoka itakuwa uzima wa milele. Tutaishi na Mungu (Warumi 8:18). Tutakuwa na Mungu milele (21:3 na Waebrania 1:12).